# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# OFISI YA RAIS

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# TAARIFA YA MAENDELEO YA UJENZI WA HOSPITALI YA WILAYA YA SERENGETI KWA MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA MHE. SAMIA SULUHU HASSAN TAREHE 06.06.2017

**OFISI YA MKUU WILAYA,**
**P. O. Box, 20,**
**MUGUMU / SERENGETI.**
**Simu Na. 0732 - 985962**
**Fax Na. 0732 - 985962**
E-mail: das.serengeti@mara.go.tz

**Juni, 2017**

## UTANGULIZI:

**Mhe, Makamu wa Rais**,

Wilaya ya Serengeti ni moja ya Wilaya zenye mvuto mkubwa kwa shughuli za Kitalii ambapo wageni wengi hufika kila mwaka kwa kujionea vivutio vya utalii vilivyopo ndani ya wilaya yetu. Wakati mwingine wageni hao wakiwa katika shughuli zao za Kitalii, huugua au kupata ajali na hivyo kulazimika kusafirishwa hadi Jijini Arusha au Nairobi Nchini Kenya ili kupata matibabu kutokana na kukosekana kwa Hospitali yenye kukidhi mahitaji yao. Nikutokana na sababu hiyo Wilaya na Mkoa zilipitisha uamuzi wa kujenga Hospitali yenye hadhi ya Kimataifa inayoweza kukidhi mahitaji ya sasa na ya baadaye kwa Wananchi wa Serengeti na wageni kutoka nje. Mpango huu wa ujenzi wa Hospitali ya Wilaya uliingizwa kwa mara ya kwanza katika Bajeti ya Serikali mnamo mwaka wa fedha wa 2007/2008.

Hata hivyo, ujenzi wa Hospitali haukuanza katika kipindi hicho (2007/2008) kama ilivyotarajiwa, kutokana na maelekezo maalum aliyoyatoa aliyekuwa Rais wa Jamhauri ya Muungano wa Tanzania Awamu ya Nne, Mhe. Jakaya Mrisho Kikwete alipofanya ziara ya Kiserikali Wilayani Serengeti. Mhe. Rais alielekeza kuwa Hospitali itakayojengwa iwe ya hadhi ya Kimataifa ili iweze kukidhi mahitaji ya Watalii wanaotembelea Hifadhi ya Taifa ya Serengeti. Kutokana na hali hiyo, Wilaya ilianza mchakato wa kumpata Mtaalamu Mwelekezi (*Consultant)* ambapo Mtaalam huyo alianza kazi, mwaka 2009 na baadaye Mkandarasi Gross Investiment Ltd. alianza rasmi ujenzi wa Hospitali hii mwezi Agosti, 2009.

## GHARAMA YA MRADI WA UJENZI WA HOSPITALI

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Kutokana na ufinyu wa bajeti mradi huu wa Ujenzi wa Hospitali ulipangwa kutekelezwa kwa awamu mbili. Awamu ya kwanza ya mradi huu ni ujenzi wa jengo la wagonjwa wa nje (OPD) na awamu ya pili ni ujenzi wa wodi za kulaza wagonjwa. Awamu ya kwanza ya ujenzi wa jengo la Wagonjwa wa nje (OPD) ulikisiwa kugharimu kiasi cha Tshs. 3,338,143,298/=. Hadi kufikia mwaka wa fedha wa 2013/2014 kiasi cha Tshs. 1,859,284,000/= zilikwishatumika. Kuanzia mwaka wa 2014/2015 hadi sasa Serikali haijaweza kutoa tena fedha kwa ajili ya mradi huu. Halmashauri ya Wilaya

Kwa mwaka 2015/2016 iliidhinishiwa kiasi cha Tshs. 270,000,000/= kati ya hizo Tshs. 200,000,000/= ni maombi maalum na Tshs. 70,000,000/= ni ruzuku ya Maendeleo (CDG), lakini fedha hizo hazikupatikana. Mwaka huu wa fedha 2016/2017 Halmashauri iliidhinishiwa jumla ya Tshs. 96,000,000/= kati ya hizo 71,000,000/= ni ruzuku ya maendeleo (CDG) na Tshs. 25,000,000/= ni mapato ya ndani lakina hadi sasa fedha hizo bado hazijapatikana.

Aidha, katika bajeti ya mwaka 2017/2018 Halmashauri ya Wilaya imeendelea kutenga kiasi cha Tshs**.** 350,000,000/=. Tshs.200,000,000/= ni kupitia ruzuku ya Maendeleo (CDG) na Tshs.150,000,000/= ni vyanzo vya ndani.

Kutokana na kukosekana kwa fedha za kukamilisha ujenzi wa mradi huu kwa kipindi kirefu, mradi ulisimama.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Uongozi wa Wilaya baada ya kuona kuwa ujenzi wa mradi huu umekwama, ulibuni mbinu mbali mbali ili kuweza kukamilisha ujenzi wa Hospitali hii awamu ya kwanza. Mbinu hizo ni pamoja na:-

(1) Kuwashirikisha wadau mbalimbali wa maendeleo kuchangia ujenzi wa Hospitali ya Wilaya.

(2) Halmashauri ya Wilaya kuendelea kutenga fedha kupitia ruzuku ya Maendeleo (CDG) na mapato yake ya ndani.

(3) Kuwa na Kamati maalum ya Usimamizi wa Ujenzi wa Hospitali yenye jukumu la kutafuta fedha kutoka vyanzo mbalimbali.

(4) Kuwashirikisha Wafanyabiashara wote wa kambi na Hoteli za Kitalii zipatazo 140 zilizopo ndani ya Hifadhi ya Taifa ya Serengeti.

(5) Kutumia kauli mbiu ya jenga Hospitali ya Wilaya kwa Sh. 1,000/=, ikiwa na maana ya kuwashirikisha Wananchi wote katika ujenzi wa Hospitali hii.

Matokeo ya juhudi hizo zilizochukuliwa na Uongozi wa Wilaya ni pamoja na kazi inayoendelea ya upigaji wa lipu majengo yote yaliyoezekwa ambayo ni jengo la Mama na Mtoto (MCH Ward), jengo la UKIMWI na Kifua Kikuu, kibanda cha Mlinzi na eneo la kusubiria la wagonjwa (Waiting Shed).

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Akaunti maalum kwa ajili ya michango ya wadau wa Maendeleo kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa Hospitali hii imefunguliwa katika Benki ya CRDB Tawi la Mugumu ili kuhakikisha kuwa fedha zote zinazopatikana zinatumika kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Akaunti hiyo inasimamiwa na Kamati Maalum ya usimamizi wa ujenzi wa Hospitali.

**JENGO LA UPASUAJI (OPERATING THEATRE)**

**Mheshimwa Makamu wa Rais,**

Serikali kupitia ufadhili wa Benki ya Maendeleoya Afrika (AfdB) imeweza Kujenga jengo la upasuaji katika mradi huu wa Hospitali ya Wilaya. Jengo hili la Upasuaji limegharimu kiasi cha Tshs. 488,000,000/=. Kwa sasa jengo hili limekamilika kwa asilimia 100 ikiwa ni pamoja na vifaa vyote vinavyohitajika.

Ili kukamilisha awamu hii ya kwanza ya jengo la wagonjwa wa nje, kiasi cha Tshs. 1,478,859,298/= zinahitajika. Wilaya inaendelea na juhudi mbalimbali za kukamilisha majengo haya ya wagonjwa wa nje (OPD) kama nilivyoeleza hapo awali. Ni matarajio yetu kuwa ifikapo Desemba, 2017 awamu hii ya kwanza ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya iwe imekamilika na huduma kuanza kutolewa.

**Mheshimiwa Makamu wa Rais,**

Kwa heshima na taadhima nakuomba utambue juhudi za wadau hawa kwa kuwakabidhi vyeti maalum ili kutambua michango yao.

**Mwisho**

Mheshimiwa Makamu wa Rais, kwa heshima na taadhima sasa nakuomba utuwekee jiwe la Msingi la ujenzi wa Hospitali yetu ya Wilaya na baada ya hapo utembelee ujenzi unaoendelea na kutupandia mti kwa ajili ya kumbukumbu.

Naomba kuwasilisha.

Nurdin H. Babu
MKUU WA WILAYA
**SERENGETI**